**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1475


# Thamani ya Ukizinda wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya Teule

**Arafa Jumanne**
*Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-05-22
Kurekebishwa: 2025-11-30
Kukubaliwa: 2025-12-07
Kuchapishwa: 2025-12-09

**Maneno Muhimu**
Riwaya
Thamani
Ukizinda
Waswahili

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Jumanne, A. (2025). Thamani ya Ukizinda wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya Teule. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(2), 108-117.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii inajadili kuhusu usawiri wa thamani ya ukizinda wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili kwa kuzingatia mifano kutoka riwaya teule. Dhana ya ukizinda huweza kutazamwa katika mielekeo mikuu mitatu. Mielekeo hiyo kwa mujibu wa Sanga (2018) na Jumanne (2025) ni mtu, vitu vya asili na sanaa. Ukizinda kama sehemu ya utamaduni wa jamii ya Waswahili, umetafitiwa zaidi katika uga wa Sosholojia (Mhlongo, 2009) kuliko katika uga wa fasihi (Jumanne, 2025). Kwa jamii ya Waswahili, ukizinda unajitokeza kama kitu chenye thamani kubwa katika utamaduni wao (Sengo, 1992). Data zinazojenga makala hii zimetokana na njia ya uchambuzi wa matini ambapo riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Harusi* (1984) zilisomwa na kuchambuliwa. Aidha, makala hii imetumia mbinu ya usimbishaji wa kimaudhui katika uwasilishaji wa matokeo huku ukiongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Matokeo ya mjadala wa makala hii yanaonesha kuwa ukizinda katika jamii za Waswahili una thamani ya namna tatu. Nazo ni: thamani ya kiutamaduni, kiteolojia na kiujumi.

## Utangulizi

Thamani ni neno linalorejelea ubora wa kitu kutokana na hali na kuhitajika kwake na jamii (TUKI, 2014). Kwa mujibu wa makala hii, neno thamani linarejelea jambo au kitu chenye hadhi ya hali inayokubalika katika jamii husika. Hali hiyo inaweza kuwa ya mwili, mali au mazingira yanayotuzunguka. Kwa makala hii tutaihusianisha na suala la ukizinda.

Ukizinda ni hali ya mwanamke kuwa na ngozi nyembamba kwenye mlango wa utupu wake (BAKIZA, 2010). Hii ni kusema kuwa ngozi hiyo hupatikana kwenye uke wa mtoto wa kike au msichana kabla ya kujamiiana na mwanamume. Fasili hii inaulenga ukizinda moja kwa moja kama ubikira. Naye Sanga (2018) anaufafanua ukizinda kuwa ni hali ya mtu, kitu/vitu, au sanaa kubaki katika uasili wake. Tukiitazama maana hii ya Sanga (2018) tunaona kuwa inauhusisha ukizinda na mambo mengine kama vile sanaa na vitu mbalimbali. Kwa makala hii, ukizinda unafafanuliwa kuwa ni ubikira, uasilia na upya katika kazi za kisanaa. Katika utamaduni wa Waswahili, ukizinda ni heshima na thamani kubwa kwa mtoto wa kike hasa katika ndoa yake. Akizungumzia suala hili Mbaabu (1985) na Sengo (1992) wanasema, ukizinda ni kitu cha thamani sana katika jamii za Waswahili kwani ndicho kitovu cha desturi yao. Kutokana na hilo, zipo hatua muhimu za kupitiwa mpaka kufikia kufunga ndoa katika jamii za Waswahili.

Kwa baadhi ya jamii za Waswahili, uamuzi wa kufanyika au kutofanyika kwa sherehe za harusi unategemea majibu ya jaribio la kupima kuwapo au kutokuwapo kwa kizinda cha mwanamke anayetaka kuolewa (Sanga, 2018). Sherehe zinaweza kuvunjika iwapo bibi harusi hatakutwa na

kizinda. Kinyume chake, ikiwa mwanamke atakutwa na kizinda, sherehe za harusi huendelea, na, wazazi na bibi harusi hupewa zawadi kutokana na matunzo, na kujitunza katika maisha (Middleton, 1992; Sanga, 2018).

Riwaya ni utanzu wenye mawanda mapana ya kusawiri maisha ya watu ukilinganishwa na tanzu nyingine. Hii hutokana na kuwa na uwezo wa kugusa vitu vionekanavyo kwa upeo wa uketo (Senkoro, 2011; Madumulla, 2022). Kwa kuwa masuala mbalimbali yanayoikumba jamii husawiriwa katika kazi za kisanaa kama vile riwaya, ushairi na tamthiliya (Mulokozi, 2017), uchunguzi ulifanywa katika riwaya teule za Kiswahili ili kudhihirisha namna ukizinda wa Waswahili ulivyo na thamani katika jamii yao.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Rosa Mistika***

Riwaya ya *Rosa Mistika* imeandikwa na Euphrase Kezilahabi. Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1971 na *East African Literature Bureau*. Utafiti uliozaa makala hii ulitumia toleo la kwanza la mwaka 1971 ambalo limechapishwa na *East African Literature Bureau*. Mwandishi wa riwaya hii anasimulia matukio mbalimbali yanayompata mhusika mkuu, Rosa, tangu akiwa mtoto hadi kufika ukubwani. Mhusika huyo alikubwa na misukosuko ambayo ilisababisha kifo chake. Fani ya riwaya hii ni ya moja kwa moja na inaeleweka kwa urahisi miongoni mwa wasomaji. Madhari yake imeundwa kwa kutumia madhari za kawaida kama vile Ukerewe, Mwanza na Morogoro ambako mhusika mkuu wa riwaya hii alipata kuishi na kusoma.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Harusi***

Riwaya ya *Harusi* imeandikwa na Abdallah Saffari mnamo mwaka 1984. Riwaya hii ilichapishwa na *African Proper Education Network*, Dar es Salaam. Toleo lililotumika katika makala hii lilipigwa chapa mwaka 2017 na *African Proper Education Network*, Dar es Salaam. Kwa jumla, riwaya inazungumzia safari nzima ya mapenzi kati ya Jane na Dakta Mustaffa. Hata hivyo, safari hiyo ya mapenzi inaingia misukosuko baada ya Wazazi wa Dakta Mustaffa kumkataa binti huyo kwa kuwa alishazaa nje ya ndoa na kuondoa ukizinda wake. Aidha, riwaya inaeleza wazo la mdogo wa Dakta Mustaffa, Rahman, kutaka kuoa, ambapo anasisitizwa na wazazi wake kuwa hawataki aibu kama ya kaka yake, Mustaffa. Riwaya imetumia lugha nyepesi na inayoeleweka kwa urahisi miongoni mwa wasomaji. Katika riwaya hiyo, kumesawiriwa mandhari kama vile Tanga Mjini na wilaya zake ambazo ni Pangani na Muheza. Vilevile, mwandishi ametuma mandhari ya Tabora, Ujerumani, na visiwa vya Komoro.

**Nadharia Iliyotumika**

Makala imeongozwa na misingi ya Nadharia ya Uhalisia katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwa sababu ndiyo iliyofaa katika kutimiza lengo la makala hii. Kwa mujibu wa Wamitila (2002) na Wafula & Njogu (2007) nadharia hii iliibuka katika karne ya 19 na hutumika mpaka leo hii katika kuchanganua kazi mbalimbali za kifasihi. Uhalisia haukuanza kama nadharia bali lilikuwa ni tapo mojawapo maarufu katika ulimwengu wa fasihi na lilikuwa na athari kubwa (Ponera, 2024). Hivyo basi, kazi zote za kifasihi zinazoangukia katika nadharia hii hazina budi kuwa akiso la maisha halisi ya jamii husika kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Wamitila (2002) anafafanua kuwa muasisi wa nadharia hii ni George Lucas (1885-1971). Uhalisia ni usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake na kuchunguza undani wa picha inayoonekana kwa uhalisi. Hivyo, msanii anatarajiwa kusawiri wahusika, na matukio yanayokubalika na kuaminika katika jamii halisi na wakati wake (Jumanne, 2016). Nadharia hii inaongozwa na misingi ifuatayo: Mosi, ni usimulizi wa kiwakati (*Mimetic Narration*). Hii ikiwa na maana kuwa kazi ya kifasihi inatakiwa kusimulia matukio kama yanavyojitokeza katika wakati husika. Pili, ni ushabihi ukweli. Katika msingi huu, kazi ya kifasihi inatakiwa ioneshe ukweli wa matukio jinsi yanavyojitokeza katika jamii husika.

Hivyo, misingi hii ndiyo iliyotumika katika makala hii kusawiri thamani ya ukizinda wa Waswahili kiutu.

**Methodolojia**

Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mbinu hii ilisaidia katika upatikanaji wa data zilizohusu usawiri wa thamani ya ukizinda wa Waswahili katika riwaya teule za Kiswahili. Mwandishi wa makala hii alisoma na kuzichambua riwaya teule ambazo ni *Rosa Mistika* (1971) na *Harusi* (1984). Riwaya hizi zilichaguliwa na mwandishi kwa sababu usomaji wa awali ulibaini kuwa riwaya hizi zimesawiri thamani ya ukizinda wa Waswahili. Hivyo, riwaya hizi ni kiwakilishi cha riwaya nyingine za Kiswahili ambazo zingesawiri thamani ya ukizinda. Baada ya kupatikana kwa data katika riwaya hizo, mbinu ya usimbaji wa kimaudhui ilitumika. Hii ikiwa na maana kuwa data zilipangwa, zikachujwa, kupunguzwa, na kudondoshwa ili kukidhi malengo ya mahitaji ya makala hii. Aidha, data ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo kwa sababu utafiti ulikuwa na mwegamo wa kitaamuli na si kitakwimu.

**Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu namna riwaya teule za utafiti uliofanyika zinavyosawiri thamani ya ukizinda wa Waswahili. Matokeo yanaonesha kuwa ukizinda wa Waswahili unabeba thamani ya namna tatu. Nazo ni: thamani ya utamaduni, teoloji na ujumi.

**Thamani ya Ukizinda katika Utamaduni**

Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani (TUKI, 2014). Hivyo, utamaduni ni mambo yote ambayo hujumuisha mifumo ya maisha kwa watu wa jamii fulani. Kila jamii ina utamaduni wake unaoendana na mila na desturi walizojipangia katika jamii yao (Khamis, 2022). Zipo baadhi ya mila na desturi zilizoandikwa katika maandishi na zipo ambazo hazijaandikwa. Zile ambazo hazijaandikwa, jamii huishi nazo kwa kupokezana kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Sera ya Utamaduni, 1997). Utamaduni ni nyenzo muhimu ya utambulisho wa jamii husika. Thamani ya ukizinda ya kiutamaduni inabainika katika maeneo mawili ambayo ni mtu na vitu vya asili vya jamii ya Waswahili.

Suala hili linabainika katika riwaya ya *Rosa Mistika* kupitia mama yake Rosa kuwa mstari wa mbele kumuusia Rosa kuhusu suala la kujitunza. Mawaidha yote haya yalitolewa kwa kuwa Rosa alitakiwa kwenda shule mbali na nyumbani kwao. Mwandishi anaeleza:

> Kwa kuwa Rosa alikuwa amekwishavunja ungo, alipewa maoni kama haya "Mwanangu, wewe sasa umekuwa mtu mzima. Karibu utakwenda huko ng'ambo Usukumani. Usitusahau sisi wazee wako tuandikie barua mara kwa mara. Jambo moja hasa ningependa kukuhadharisha wavulana wakorofi. Huenda wakakutaka mapenzi, nia yao ikiwa tu kukupa mimba itakayokatisha masomo yako. Daima wakwepe hao (uk. 11).

Dondoo hili linafafanua namna wazazi wanavyotamani watoto wao wasiharibikiwe katika maisha yao. Hili linatokana na sababu kuwa wao ndiyo wenye jukumu kubwa la kuwalinda na kuwaeleza ukweli kuhusiana na maisha. Wosia huo hutolewa kwa mtoto wa kike kwa sababu hatakuwa tena karibu na wazazi wake kwa wakati huo. Huu ndiyo utamaduni wa jamii za Waswahili ambao unasawiriwa katika kazi za kifasihi. Suala hili la thamani ya ukizinda kiutamaduni imesawiriwa katika riwaya hii kwa sababu msingi wa kwanza wa Nadharia ya Uhalisia unamtaka mtunzi kutunga kwa kuzingatia ushabihi ukweli. Hii ni kwa sababu thamani hiyo hujitokeza katika jamii ya Waswahili na mtunzi akaamua kuandika katika kazi yake ya kifasihi kama inavyosawiriwa katika jamii yake. Akizungumzia suala la thamani ya ukizinda katika utamaduni, Mbaabu (1985) anasema

kuwa ukizinda ni mila na desturi inayopewa thamani sana katika jamii za Waswahili kama sehemu ya utamaduni wao.

Katika riwaya ya *Harusi*, suala hili la thamani ya ukizinda katika utamaduni linajitokeza kupitia wazazi wa Rahman ambao walihangaika kumtafutia kijana wao mwanamke ambaye alikuwa na kizinda ili kulinda thamani hiyo ya kiutamaduni kama sehemu ya mila na desturi za Waswahili. Mwandishi anaeleza:

> "…Weye sema tu baba", Alhaji alimtia mdadi, akaendelea, "maana sisi sio wachochole. Tumezagaa Pwani na Mrima," Aligea mkono kuonesha pande mbalimbali, akaendelea, "wako babizo na mamizo Comoro, Pemba, Mwambao wote, Unguja, Tanga. Na wapi tena?" Alimwangalia mkewe kumtaka msaada, ambaye alidakia kwa shauku, "Naam, Mafia, Kigoma, Kilwa na …"
>
> Waona basi na kote huko ni kiasi cha kuagiza tu mambo yawa" (uk. 54).

Dondoo hili linaonesha thamani ya ukizinda kiutamaduni, kwani wazazi wanaonesha shauku ya kumtafutia mtoto wao mchumba ambaye wanaamini amekulia na kulelewa katika familia inayoeleweka kimaadili. Akifafanua kuhusu hoja hii, Farsy (1956) anatoa mfano wa watu wa Unguja, namna wanavyofuata desturi hii kukamilisha shughuli nzima ya harusi. Tumekwishajadili katika sehemu ya utangulizi kuwa ukizinda wa Waswahili unasawiriwa katika riwaya teule katika maeneo ya mtu, vitu vya asili, na sanaa. Thamani ya ukizinda katika utamaduni inapatikana pia katika jamii za Waswahili kwa kupenda vitu vyao vya asili.

Utamaduni wa Waswahili unaambatana na vitu vyao vya asili, hasa katika chakula, vinywaji na vitu vingine vya kimatumizi. Waswahili hupendelea kula vyakula kama vile mihogo, viazi, na magimbi ambavyo vimo katika asili yao. Aina hii ya mazao hutumika kutengeneza vyakula mbalimbali vya asili kama vile *kishumba*, *bada*, na *mseto*. Vyakula hivi vilitumiwa kwa wingi katika mazingira na maisha halisi ya Waswahili ili kuleta siha katika miili yao (Wizara ya Afya, 2023).

Riwaya teule za makala hii zimesawiri thamani ya ukizinda kiutamaduni kupitia riwaya ya *Rosa Mistika* na *Harusi* ambapo familia ya Zakaria na Alhaji Mwinyi Karimu zilikuwa zinakula na kutumia vyakula vya asili ya Waswahili katika milo yao mikuu kwa siku. Miongoni mwa vyakula hivyo vya asili ni mihogo, viazi, ugali, nazi, ndizi, mahindi, choroko, mbaazi, na kunde. Mwandishi wa *Rosa Mistika* anaeleza: "Regina alikuwa amekwishachimba viazi wakati Zakaria alipokusanya nguo kuukuu za kaniki (uk. 10)… "Flora alikuwa amekwishapakua ugali (uk. 11)." Nukuu hizi zinaonesha namna Waswahili wanavyothamini na kutumia vyakula vya asili yao kama sehemu ya utamaduni wao.

Vilevile, katika riwaya ya *Harusi* mwandishi anafafanua vyakula vya asili vilivyotumiwa na Alhaji Karimu. Anasema:

> … Pangani ni maarufu kwa rutuba unayoileta na kuitupa kwenye kingo zake pana ambako mashamba ya migomba, popoo na minazi nawanda na kustawi ajabu… Migomba ilisukuma mikungu iliyojikokota ardhini, baadhi yake ikawa imekomaa mno na kuanza kuivisha ndizi zake, kote kukasikika harufu bora ya ndizi mbivu za malindi, kupusa, kisukari, mbali na mkono wa tembo na mabokoboko … huku wakijilimia maeneo madogo ya kutosha mahitaji yao ya mihogo, mahindi, kunde, choroko, mbaazi na kadhalika (uk. 27).

Dondoo hili linabainisha namna jamii za Waswahili zinavyotumia vyakula vyao vya asili kama sehemu ya utamaduni wao. Utumiaji wa vyakula hivyo katika jamii za Waswahili ni thamani kwa

sababu vyakula hivyo vipo katika utamaduni wa Waswahili. Suala hili linatiliwa mkazo na Nadharia ya Uhalisia kwa kupitia msingi wake wa kwanza kwa sababu mtunzi ametumia ushabihi ukweli wa hali halisi ya maisha ya jamii ya Waswahili. Hii ni kwa sababu vyakula hivi kweli vinapatikana na kutumiwa kwa wingi katika jamii hiyo. Pia, familia hizi za Zakaria na Alhaji Karimu zilikuwa zinatumia vifaa vya kimatumizi vya asili kama ilivyo kwa asili ya Mswahili kutumia vitu vya utamaduni wa wao. Vitu kama vyungu, mikuki, karabai, na vyombo vya usafiri wa majini (mashua na majahazi) ni utamaduni wa Waswahili katika matumizi yao ya kila siku. Vifaa hivyo vya asili vya kimatumizi vinaweza kutumika katika kupikia na silaha za kujilinda katika familia.

Suala hili linathibitika katika Riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anamuonesha Zakaria alivyotumia silaha aina ya mkuki wakati akimfuata Charles nyumbani kwao. Anasema "Katikati ya mji alisimama Zakaria pamoja na bintiye, mkuki mkononi" (uk. 7). Kinachoonekana hapa ni silaha aina ya mkuki na inavyotumiwa na watu katika jamii za Waswahili. Haya yote yanasawiriwa katika riwaya teule na kushadidiwa na misingi ya Nadharia ya Uhalisia kwa sababu mtunzi hutakiwa kuonesha uhalisi wa kile kinachotokea katika jamii yake ingawaje anaweza akaweka ubunifu katika kazi husika.

**Thamani ya Ukizinda katika Teolojia**

Teolojia ni taaluma ya tabia na sifa za Mungu na misingi ya imani za dini (TUKI, 2014). Neno teolojia limetumika kumaanisha elimu itolewayo kuhusiana na masuala ya dini. Utafiti umebaini kuwa ukizinda katika riwaya ya Kiswahili unafafanua thamani ya kidini kupitia riwaya teule za makala hii. Dini ni njia muhimu inayoaminiwa sana ya kulinda ukizinda kwa mwanamke kama thamani inayopaswa kutunzwa mpaka siku atakapoingia katika ndoa na mume wake. Tafiti zinaonesha kuwa thamani ya ukizinda ya kidini hupunguza uzinzi na kujilinda kwa wanawake (Rostosky & Wenzake, 2003; Randall, 2004; Sinha, 2007). Thamani ya kidini inayosawiriwa inatokana na *Kurani* na *Biblia*, hasa katika kipengele cha ubikira. Vitabu vitakatifu vinaonesha thamani ya ukizinda ya kidini kama sehemu ya maadili ya dini husika, hasa katika suala la ndoa kwa mwanamke na mwanamume.

Dini za Uislamu na Ukristo zinathamini ukizinda kama sehemu ya maadili yake. Katika dini ya Uislamu, kwa mfano, wasichana wanafundishwa na kusisitizwa kutunza vizinda kabla ya ndoa kama maandiko matakatifu ya *Kurani* yanavyosema. Katika kuthibitisha thamani ya ukizinda katika teolojia katika dini ya Uislamu, mwandishi wa riwaya ya *Harusi* anaonesha namna wazazi wa Dakta Mustaffa walivyochukizwa na taarifa ya kijana wao kuoa mwanamke ambaye hana kizinda na alishazaa kabla ya ndoa. Anaeleza:

> "Sasa mama umeshampata, yaani mchumba? …"
>
> "Ninaye. Anaitwa Jane… Na sipendi kuwaficha kuwa ameshazaa binti mmoja …" Dakta Mustaffa hakupenda kumpa adhabu baba yake kwa maudhi ambayo yangechamua ugonjwa wa moyo. Lakini ngoma alishaanza kuipiga ilibidi aicheze.
>
> "Sasa mimi nakata shauri. Kama kweli mimi babiyo huna ruhusa kufanya hivyo, na ukome …" (kur. 37-38).

Dondoo hili linafafanua jinsi baba yake na Dakta Mustaffa asivyoafiki mtoto wake kumuoa Jane. Mzee Alhaji anamkatalia mtoto wake kuoa mwanamke ambaye ameshazaa kwa sababu kwa mafundisho ya dini ya Uislamu hana sifa ya kuolewa kutokana na kukosa kizinda. Kitendo cha Dakta Mustaffa kumtambulisha mchumba aliyezaa kabla ya ndoa ni kinyume na desturi hiyo.

Katika dini hiyo ya Uislamu, wasichana wanasisitizwa, wanahimizwa, na kufundishwa kutunza bikira (Sinha, 2007). Suala hili linathibitishwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisia ambao humtaka mtunzi kutunga kulingana na wakati uliopo. Hii ni kwa sababu katika zama hizi imeonekana kuwa vijana hawaupi ukizinda kipaumbele.

Hoja hii ya thamani ya ukizinda kiteolojia inafafanuliwa na Al-Ghazzali (hakuna mwaka) ambaye anasema: "Kuoa mwanamke mwenye kizinda ni kwa sababu mwanamke huyo humpenda mume wake kutokana na alivyomzoea. Hii ni kwa sababu kimaumbile mtu humzoea mwanamme wa kwanza zaidi kuliko wa pili" (uk. 52). Dondoo hili linafafanua wazi kuwa ukizinda una nafasi kubwa ya kulinda na kudumisha ndoa pamoja na malezi ya watoto katika jamii za Waswahili. Hata dini zao wanazoziamini na zinasisitiza sana kuulinda ukizinda.

Maoni hayo kuhusu wanajamii kujiepusha na zinaa kabla ya ndoa (kuoa au kuolewa kwa mwanamume au mwanamke mtawalia) yanatiliwa nguvu na aya ya tatu ya sura ya ishirini na nne ya *Kurani* (24:3) ambayo inasema: "Mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina" (Al-Farsy, 1991). Hii ikiwa na maana ya kuwa mtu mzinifu humpata mwenza ambaye ni mzinifu pia; na kama sio mzinifu basi atapata mwenza asiye mzinifu. Aya hii ina mafunzo na maonyo; hivyo husaidia jamii kuishi katika maadili.

Kwa upande wa dini ya Ukristo, ukizinda pia una thamani kubwa. Utafiti ulibaini kuwa nembo inayosimama kama kielelezo muhimu cha thamani ya ukizinda katika dini hii ni sifa inayoambatana na jina la Maria ambaye ni mama wa Yesu. Katika kuonesha taadhima ya kiwango cha juu, jina la Maria hutamkwa kwa kutanguliziwa sifa ya ubikira, yaani huitwa Bikira Maria. Kwa kawaida, watu katika jamii nyingi hapa duniani hutambuliwa kwa majina mawili au matatu. Kwa maoni yetu, sifa hiyo ya ubikira kwa Maria imechukua nafasi kubwa kiasi hata cha sehemu kubwa ya waumini wa dini hiyo kutojua jina kamili la mama huyo, ambaye, kwa mujibu wa *Islamic Propagation Centre* (2007), ana heshima kubwa katika dini zote kubwa zinazoaminiwa na jamii mbalimbali za Waswahili (Ukristo na Uislamu).

Tunaamini kuwa mwandishi Kezilahabi, katika riwaya ya *Rosa Mistika*, ametumia jina la Rosa Mistika ili kujenga mwigo wa kisanaa kuhusu heshima ya ubikira katika uga wa kiteolojia—akihusisha ruwaza ya jina hilo la mhusika wake mkuu na ruwaza ya jina la Bikira Maria. Anamfunulia msomaji wake kuhusu undani wa jina hilo kupitia mwelekeo wa ubwege wenye ufutuhi. Maudhui haya yamo katika majibizano yanayofanyika getini kati ya Rosa na walinzi wa shule aliyokuwa anasoma Flora, mdogo wake. Mwandishi anasema:

> "Jina lako nani?" Yule polisi alimuliza.
> "Rosa."
> "Rosa nani?"
> "Rosa Mistika."
> "Mistika ndio baba'ko?"
> "Hapana, Zakaria."
> (kur. 6-62).

Haya ni maswali ya msingi ambayo, kwa maoni yetu, mwandishi anataka wasomaji wake walitafakari jina la mhusika wake kwa undani. Ponera (2014) anaeleza kuwa Kezilahabi amesuka maswali haya katika namna ya kibwege kwa makusudi ili kuiamsha akili ya msomaji kuhusu jina kamili la mhusika mkuu wa riwaya hii, Rosa, ambaye toka mwanzo wa riwaya hatajwi kwa kutumia u-bini wa Zakaria. Ponera (2014) anaongeza kuwa msikiko wa 'Rosa Mistika', kwa juujuu, uko kama vile ni majina mawili, yaani, la Rosa mwenyewe na la baba yake.

Kwa ujumla, dhana ya ukizinda katika muktadha wa dini ya Ukristo huonesha utakatifu, ambapo mwanamke bikira hupata heshima na kuthaminiwa katika jamii yake. Ukizinda katika dini ya Ukristo ni ishara ya maadili mema, kujitunza, na kuleta thamani katika familia kama jinsi maandiko ya *Biblia* yanavyosisitiza, kuelimisha, na kuhamasisha. Ukizinda katika Ukristo unahusu utakaso ambao unapaswa kuathiri moyo, akili, na nafsi na si tu sehemu fulani za mwili. Msisitizo wa *Biblia* si juu ya ufafanuzi wa kina wa bikira kama ilivyo katika hali ya moyo wa mtu. *Biblia* ipo wazi kusisitiza thamani ya ubikira. *Biblia* (1997) inasema "Basi watumishi wa mfalme waliomuhudumia walimwambia, Mfalme na atafutiwe mabikira vijana wazuri" (Esta 2:2). Hii inamaanisha kuwa kitendo cha watumishi hao kusisitiza mfalme atafutiwe vijana mabikira kinaonesha ubikira una thamani kubwa katika dini ya Ukristo.

Katika kulifafanua suala hili la thamani ya ukizinda katika teolojia, mwandishi wa riwaya ya *Harusi*, kupitia dini ya Ukristo, anawatumia Dakta Mustaffa na Jane. Dakta Mustaffa anamfafanulia Jane kosa alilolifanya kwa wazazi wake kwa kuzaa kabla ya ndoa, kinyume na dini ya Ukristo inavyofundisha na kusisitiza. Anaeleza:

> … Basi yeye anahisi umemtia aibu na kumtoa thamani kabisa mbele ya wazee wenzake. Labda mngekuwa madhehebu ya Lutherani au mengine mambo yangekuwa tafauti. Nasikia kuwa nyie Wakatoliki mnajali sana mambo ya bikira, na kadhalika… Baada ya muda mrefu, Dakta Mustaffa aliendelea, Sishangai kuona baba yako amekasirishwa kiasi hicho, pengine ni mapema mno kumtaka asahau matumaini makubwa mno aliyokuwa nayo kwako kumpatia mkwe kwa njia inayoambatana na taratibu zote za dini yenu. Si umenieleza kuwa yeye ni mmoja wa wazee wa kanisa (uk. 13).

Dondoo hili linasisitiza kuwa misingi ya Ukristo inaeleza kuwa ni lazima ukizinda utunzwe sana kabla ya kuingia katika ndoa takatifu kati ya mwanamke na mwanamume. Mwanamke asiguswe na mwanamume yeyote yule kabla ya ndoa. Kwa kufanya hivyo, mwanamke atakuwa anatenda kile alichoamrisha na kukisisitiza Mwenyezi Mungu katika maandiko yake matakatifu. Nadharia ya Uhalisia inalithibitishasuala hili kwa kupitia msingi wake wa ushabihi ukweli kwani huu ndio ukweli unaopatikana katika jamii za Waswahili kuhusiana na thamani ya ukizinda katika teolojia na kusawiriwa katika kazi za kifasihi.

Vilevile, matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa ukizinda katika dini ya Ukristo ni agano. Mara nyingi, agano huhusishwa na damu. Kwa kuwa mara nyingi mwanamke anapotolewa kizinda kwa mara ya kwanza hutoka damu, basi huwa agano kati yake na mumewe. Kutokana na hili, huwa vigumu mwanamke kumsahau mwanamume aliyemtoa bikira katika maisha yake.

Riwaya ya *Harusi* inathibitisha suala la kuwa ukizinda ni agano kupitia mhusika Jane. Mwandishi wa riwaya hii anatuonesha kuwa Jane hakumsahau hawara yake wa kwanza ambaye alitoa ubikira wake. Mwandishi anaeleza:

> Wazo la kuanguka kwa matiti hayo sababu ya uzazi halikumwudhi sana Jane, maana uzazi masika, ugumba kiangazi. Isipokuwa tu kitendawili cha mimba ya Jane bado hakupata kukitegua, daima akahisi dhahiri dunia imemchezea shere, au labda, kwa usahihi zaidi, mwalimu wake, Alfred Mkali, huko Chuo cha Uhazili Tabora alimzidi mbinu. Fikra hizo ambazo alijaribu kuzizuia, ziliyongayonga na kunata akilini mwake zikamsusia kuondoka kabisa. Wajihi mbaya wa Alfred Mkali katu usiolingana hata tumba na haiba ya Jane, hata kwa sasa, wachilia mbali miaka mitano iliyopita, uliambatana na mawazo hayo daima na kumchefua moyo zaidi. Na kama vile yote hayo hayakutosha kumtonesha

> jeraha la moyo ile siku ambayo alifanya mapenzi na Alfred Mkali aliyeitwa sokwe hapo chuoni kwa jina la utani iliandamana tena na mawazo yake yakaufanya moyo urindime zaidi kwa uchungu (uk. 5).

Kinachofafanuliwa na dondoo hili ni kuwa ukizinda ni agano kati ya mwanamke na mwanamume. Agano hilo hufanyika wakati mwanamume na mwanamke wanaposhiriki tendo la ndoa na kutoa kizinda. Kwa kufanya hivyo, inakuwa ngumu msichana kumsahau mvulana wake wa kwanza. Dondoo hili linaonesha miaka mitano imepita lakini Jane bado anamkumbuka mpenzi wake wa kwanza aliyemtoa usichana wake. Hii ni kwa sababu aliamini kuwa atakuwa naye mpaka watakapofunga ndoa. Kusawiriwa kwa suala la kutomsahau mpenzi wa kwanza katika dondoo hili kunarejelea agano na kusistizwa na Nadharia ya Uhalisia ambayo humtaka mtunzi kushadidia ukweli unaopatikana katika jamii yake.

**Thamani ya Ukizinda katika Ujumi**

Ujumi ni tawi la falsafa linalojishughulisha na uzuri, ubaya, ladha ya mambo au vitu mbalimbali, pamoja na uchanya na uhasi wa kazi ya kifasihi (Sanga, 2012, 2018; Badru, 2015). Makala hii inafafanua thamani ya ujumi kwa mwanamke, hasa katika ukizinda wake. Hapa tunamaanisha kwamba thamani ya ukizinda kiujumi hufafanuliwa katika uzuri wa mtu (mwanamke). Uzuri huo unaweza usibainike katika utu lakini ukamheshimisha kwa jamii yake. Thamani ya ukizinda katika ujumi kwa mtu inapatikana kwa mwanamke mwenye kizinda. Katika jamii za Waswahili, mwanamke mwenye kizinda ndiye huonekana mzuri ikilinganishwa na asiyekuwa nacho (Mbiti, 2000). Hii ni kutokana na idili za jamii yao.

Jambo hili linasawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* pale ambapo Zakaria alitaka mwanawe, Rosa, awe na thamani hii ya kiujumi pindi atakapoolewa na mume wake. Kutokana na hili, alikuwa mkali na hata kumzuia Rosa asichangamane na wanaume ili wasije wakamuharibia thamani hiyo ya kiujumi. Rosa aliwaogopa wavulana kiasi hata cha kutochangamana nao ili kutunza thamani ya kizinda chake kama baba yake alivyotaka. Mwandishi anaeleza:

> … Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa, hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na babake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote. Na Zakaria alipojua hayo alifurahi sana. Alijidai kwamba yeye alifahamu jinsi ya kulea binti zake, hasa alipokuwa amekunywa kidogo … Kutokana na namna hii, Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu asiopaswa kuandamana nao, au hata kuzungumza nao. Alianza kufikiri kwamba alitakiwa kujitosheleza. Alizidi kuwa mnyamavu (uk.7).

Dondoo hili linathibitisha namna ya kulinda kizinda ili kupata thamani ya kiujumi. Msichana hutakiwa kutunza kizinda chake ili aonekane ni mzuri katika jamii za Waswahili. Hoja hii inaungwa mkono na Mbiti (2000) na Kamage (2023) ambao wanafafanua thamani ya ukizinda ya kiujumi, hasa kwa mtu inatokana na kutunza kwake ukizinda wake hadi siku atakapoolewa.

Kwa upande wa riwaya ya *Harusi*, thamani ya ukizinda katika ujumi imesawiriwa kwa namna tofauti kupitia wazazi wa Rahman. Kwanza, walikataa mtoto wao, Dakta Mustaffa, kuoa mwanamke ambaye hana kizinda kwa kuamini kuwa siyo mzuri kutokana na mila na desturi zao. Pili, walimchagulia kijana wao, Rahman, msichana mwenye kizinda ili kulinda thamani hiyo ya kiujumi kama ilivyo kwa jamii za Waswahili. Kwa jamii yao, mwanamke mwenye kizinda ndiye mzuri. Mwandishi anaeleza: "Miye na shangazilo tulikuwa tumevutiwa na kisichana kizuri cha haja, katoto cha watu huko ushongo. Sasa baba yawa watusikia, tufanye mipango twende huko ukamwone taraa utampenda" (uk. 39). Kwa kutumia dondoo hili, ni wazi kuwa jamii za Waswahili zinathamini mwanamke mwenye bikira pindi kijana anapotaka kuoa. Ndiyo maana wazazi

huvutiwa na wasichana wazuri wenye kutunza ukizinda wao. Kwa upande wa wazazi wa msichana mwenye sifa hiyo, hupewa hongera nyingi.

Akiunga mkono suala la kuthaminiwa kwa msichana anayeolewa huku akiwa na kizinda, kama sehemu ya uzuri wake Maitaria (2019) anasema kuwa posa na sifa za wasichana bikira huvuma karibu na mbali zaidi kuliko wasiokuwa na bikira. Anakazia suala hili kwa kutoa methali isemayo "Chema chajiuza, kibaya chajitembeza". Suala hili linaumana na msingi wa kwanza na wa pili wa Nadharia ya uhalisia inayositiza mtunzi kutunga kwa kuzingatia ushabihi ukweli na utunzi wa kiwakati. Thamani hizi tulizozijadili ndizo zinazosawiriwa katika maisha halisi ya jamii za Waswahili.

**Hitimisho**

Suala la ukizinda katika jamii za Waswahili hutazamwa kama kitu chenye thamani na hupewa kipaumbele katika jamii ya Waswahili. Jambo hili linatokana na ukweli kuwa hata katika maandiko matakatifu yasisitiza kutunza thamani hii ya ukizinda ambayo haipaswi kuharibiwa mpaka ndoa. Hii ni kusema kuwa mtoto wa kike hutakiwa kujitunza kwa hali na mali ili asiiharibu thamani hiyo. Hivyo, msisitizo mkubwa wa ukizinda umewekwa kwa wanawari kulinda ukizinda wao na hasa kuacha kufanya mapenzi kabla ya kufikia muda wa ndoa. Hii itasaidia kuingia katika ndoa wakiwa na ukizinda ili wawe na thamani ya ukizinda. Makala inapendekeza kuwa jamii ya Waswahili iendelee kuuthamini ukizinda kwa sababu ni kitu ambacho kinaweza kuimarisha utamaduni wa jamii ya Waswahili. Thamani hii ya ukizinda inapaswa kutunzwa na wanawake na wanaume. Hii itasaidi zaidi kudumisha utamaduni unaotambulisha jamii ya Waswahili.

**Marejeleo**

Al-Farsy, A. S. (1991). *Kurani Takatifu*. The Islamic Foundation.
Al-Ghazzali, A. H. (hakuna mwaka). *The Beginning of Guidance* (*Bidayat al-Hidaya*). White Thread Press.
Badru, Z. (2015). *Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vya Kiswahili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili* (Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma).
BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press. Co. Ltd.
Chama cha Biblia Tanzania (1997). *Biblia*. The Bible Society of Tanzania.
Farsy, M. (1956). *Ada za Harusi katika Unguja*. East African Literature Bureau.
Islamic Propagation Centre (2007). *Elimu ya Dini ya Kiislamu - Madrasa na Shule za Msingi: Kitabu cha Saba*. Islamic Propagation Centre.
Jumanne, A. (2016). *Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya za Shaaban Robert na Said. A. Mohamed* (Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma).
Jumanne, A. (2025). Usawiri wa Ukizinda kwa Mawanda ya Mtu katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Rosa Mistika* na *Harusi*. *Nuru ya Kiswahili*, 4(1), 58-85. Inapatikana katika https://doi.org/10.58548/2024nuru41.5885.
Kamage, A. (2023). Usawiri wa Nguvu-uhai katika Jamii za Kiafrika: Mifano kutoka katika Riwaya ya "*Mzishi wa Baba Ana Radhi*". *Mwanga wa Lugha*, 8(1), 37-48.
Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. East African Literature Bureau.
Khamis, T. (2022). *Mdhihiriko wa Ontolojia ya Wazanzibari katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla* (Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma).
Madumulla, J. S. (2022). *Riwaya ya Kiswahili*: *Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Afroplus Industries Limited.

Maitaria, J. (2019). Methali za Kiswahili kama Wenzo wa Kubainishia Falsafa ya Kiafrika kuhusu Familia. Katika A. S. Ponera na Z. A. Badru, (Wah.) *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Prof. Madumulla* (Kur. 435-456). Karljamer Publishers Ltd.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili. Isimu Jamii*: *Nadharia na Mukktadha wa Kiswahili*. Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Mbiti, J. (2000). *Introduction to African Religion* (2nd Ed). East African Educational Publishers Ltd.

Mhlongo, P. (2009). *Reasons for Undergoing Virginity Testing: A study of Young People in Rural Kwa Zulu-Natal, South Africa* (MA Thesis, Chuo Kikuu cha South Africa).

Middleton, J. (1992). *The World of the Swahilian African Mercantile Civilisation. New Heaven*. Yale University Press.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU.

Wafula, R. & Njogu. K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Ponera, A. S. (2014). *Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi* (Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma).

Ponera, A. S. (2024). Riwaya ya *Rosa Mistika*: Kurunzi ya Malezi ya Vijalunga. *Nuru ya Kiswahili*, 3(1), 43-69.

Randall, C. (2004). *Interaction Ritual Chains*. Princeton University Press.

Rostosky, S., Riggle. E., Gray, B., & Hatton, R. (2003). Minority Stress Experiences in Committed Same-Sex Cauple Relatioship. Journal of Adolescence, 38(4), 392-400. https://10.1037/0735-7028.38.4.392.

Saffari, A. (1984). *Harusi*. African Proper Education Network.

Sanga, A. (2012). *Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa Muhammed Said Abdulla na Aristablus Elvis Musiba* (Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma).

Sanga, A. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano kutoka Magazeti ya Habari Leo, Nipashe na Mwananchi* (Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma).

Sengo, T. (1992). Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja. *Nordic Journal of African Studies* 1, 53–79.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam University Press.

Sinha, R. (2007). The Role of Stress in Addiction Relapse. *Current Psychiatry Reports*, 9(1), 388-395. Inapatikana katika https://doi.org/10.1007/s11920-007-0050-6.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. TUKI.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Phoenix Publishers Ltd.

Wizara ya Afya (2023). *Mwongozo wa Chakula na Ulaji Tanzania Bara: Ushauri wa Kitaalamu*. Wizara ya Afya.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997). *Sera ya Utamaduni*. Mwananchi Publisher.